# MWONGOZO WA VYOMBO VYA HABARI KATIKA KUANDIKA

# HABARI ZA WATOTO

BARAZA LA HABARI TANZANIA (MCT)

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA (MCT)

(BARAZA LA HABARI TANZANIA)

# MWONGOZO WA VYOMBO VYA HABARI KATIKA KUANDIKA HABARI ZA WATOTO

MWONGOZO WA VYOMBO VYA HABARI
KATIKA KUANDIKA HABARI ZA WATOTO

© Media Council of Tanzania, 2022

ISBN: 978-9976-588-00-2

# YALIYOMO

**SEHEMU YA 1: UTANGULIZI**........................................................1

**AZIMIO**......................................................................................2

**SEHEMU YA 2: TAFSIRI** .......................................................................4

**SEHEMU YA 3: MASLAHI YA MTOTO** .......................................5

**SEHEMU YA 4: HAKI NA WAJIBU WA MTOTO** ........................9

**A. HAKI ZA MTOTO**............................................................................9

**B. WAJIBU WA JUMLA WA MTOTO**........................................ 10

**SEHEMU YA 5: MIONGOZO YA MAADILI NA KANUNI** .. 11

**Rejea** .......................................................................................... 17

# SEHEMU YA 1: UTANGULIZI

Changamoto ya kila siku kwa wanahabari imekuwa ikijidhihirisha zaidi katika kuandika habari za watoto na haki zao. Watoto wanahitaji uangalizi maalum na ulinzi kwa sababu ni kundi lililopo hatarini. Hata hivyo, mara nyingi waandishi wa habari za watoto wamekuwa wanawajengea taswira hasi, hivyo kuwaweka katika hatari ya kuhukumiwa kimakosa au kunyanyapaliwa na jamii.

Kupitia uandishi wa habari za watoto, vyombo vya habari vinaweza kushawishi na kuwakumbusha watunga sera na umma kwamba, watoto nao ni binadamu wanaostahili kutambuliwa, kupewa hadhi, heshima na zaidi ya yote, kulindwa.

Kwa hiyo kujenga uandishi wenye uelewa, umakini na weledi ni jambo muhimu kwa kila chombo cha habari ili kuboresha uandishi wa habari za watoto na kulinda usalama wao kimwili na kihisia.

Katika kufikia lengo hilo, Baraza la Habari Tanzania linaweka kanuni, maadili na miongozo, kwa lengo la kuleta mwamko juu ya haki za watoto miongoni mwa wanahabari.

Zaidi ya hayo, miongozo hii inalenga kuwawezesha wanahabari kuandika kwa ufanisi habari zinazohusu watoto; kwa namna ya mwitikio zaidi na kitaalamu na kwa kufuata ipasavyo kanuni na maadili; kuelimisha watu na kushawishi uamuzi wa jamii katika masuala yanayoathiri ustawi wa mtoto.

"Miongozo mizuri haizungumzii mambo 'halali' na 'haramu' tu, bali huweka wigo wa kutafakari masuala ya maadili" Haki za Watoto IFJ (2002)

Baraza la Habari Tanzania linaamini mwongozo huu siyo tu kwamba utaangalia mambo ya kufanya au kutofanya, bali pia utaviwezesha vyombo vya habari kuwa sauti ya watoto, kuchunguza udhalilishaji na unyanyaswaji wao kuongeza mwamko zaidi wa umma na watunga sera kuhusu watoto, kubadili

mitazamo na hatimaye kukomesha ukiukwaji wa haki za watoto.

## AZIMIO

Sisi waandishi wa habari, wanataaluma ya habari, wapiga picha za mnato, waandishi wa makala maalum, watangazaji wa redio na televisheni, wachapishaji wa mitandaoni na wapiga picha za video;

## Kwa kutambua kwamba:

- vyombo vya habari vina nyenzo na uwezo wa kuweka haki za watoto katika ajenda ya habari,
- katika kuandika habari, lengo lazima liwe kutetea maslahi mazuri kwa mtoto,
- watoto wanastahili kuwa na jukwaa la kutoa maoni yao kuhusu masuala yanayowagusa,
- watoto wanayo haki ya kulindwa wasiumizwe au kupatwa na aina yoyote ya madhara,
- kimsingi, watoto wana mahitaji sawa, hadhi na haki kama watu wazima.

## Kwa hiyo basi, mwanataaluma wa habari atapaswa:

- KUPIGANIA kudumisha viwango vya juu vya maadili ya kuandika habari;
- KUANDIKA habari ambazo kila wakati zitakumbusha na kuhamasisha umma kupigania haki za watoto; kusaidia makuzi na maendeleo yao na kuwalinda dhidi ya habari yoyote au picha zinazokuza unyanyasaji wa kijinsia, ukatili, matumizi haramu ya dawa za kulevya na migogoro.
- KUJIZUIA kuandika habari au kutumia vielelezo, picha au michoro inayowaweka watoto katika hali ya hatari au udhalilishaji;
- KUEPUKA kutumia maneno yanayobagua, kuleta unyanyapaa na mshituko kwa watoto;

- KUEPUKA kutoa maelezo yatakayosababisha kumuweka mtoto katika hali ya dhalili, kuleta madhara ya kimwili na kisaikolojia au manyanyaso ya muda mrefu, ubaguzi na kukataliwa na jamii yake;
- KUPATA ridhaa ya maandishi kutoka kwa watoto wenyewe kupitia kwa wazazi wao, wahusika wakubwa/waangalizi ama walezi, kabla ya mahojiano na watoto au kuwapiga picha;
- KUWA na uvumilivu na umakini unapohoji watoto, kwa katumia maneno au lugha wanayoielewa kwa wepesi zaidi;
- KUEPUKA kusambaza mitandaoni picha zinazodhalilisha watoto au kuwaweka katika mazingira hatarishi;
- KUHESHIMU watoto wote bila kujali jinsi, kabila, ulemavu, hali zao za kiuchumi au wawe wanaishi vijijini au mijini;
- KUTAFUTA maoni ya watoto. Shawishi upatikanaji wa fursa ya kuweka habari za watoto katika vyombo vya habari na kukuza haki yao ya kusikilizwa na kushiriki katika uamuzi wa masuala yanayowahusu;
- KULINDA utambulisho wa watoto wakati wa kuandika habari kuhusu masuala nyeti yanayoweza kufanya watambulike. Kila wakati hakikisha usalama na faragha ya watoto, wawe waathirika wa matukio, mashahidi au wahalifu;
- KUFIKIRIA athari za kuchapisha habari zinazohusu watoto; kuficha utambulisho wao isipokuwa tu kama utamsaidia mtoto na ni kwa manufaa ya umma.

# SEHEMU YA 2: TAFSIRI

- **Mtoto:** Ni mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane (18). Hii ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 na Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto wa mwaka 1989 na mikataba mingine ya kimataifa.
- **Mlezi:** Ni mtu anayemwangalia au kumsimamia mtoto, au mtu aliyeteuliwa kwa mkataba, wosia au amri ya mahakama kwa kupewa dhamana ya kuangalia na kutunza mali na haki za mtoto.
- **Mzazi:** Baba au mama mzazi, baba au mama wa kambo na mtu mwingine mwenye dhamana ya kumwangalia mtoto.
- Kwa madhumuni ya mwongozo huu, wanataaluma wa habari wanaozungumziwa ni wale wote wanao husika kwenye uchapishaji au utangazaji wa habari magazeti, radioni, luninga na mitandao ya kijamii.
- Hawa ni waandishi wa habari binafsi, wakusanya habari, wahariri, waandishi wa makala maalum kwenye magazeti na mitandao ya kijamii, wachora vikaragosi/katuni, wapiga picha za mnato, wapiga picha za video, watangazaji wa radio na televisheni na watayarishaji  wa vipindi.

# SEHEMU YA 3: MASLAHI YA MTOTO

"Kwenye mambo yote anayotendewa mtoto na watu binafsi au mamlaka, maslahi ya mtoto lazima yawekwe mbele." Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, (1999).

Hivyo basi, katika kuandika habari kuhusu watoto, wanataaluma ya habari hawana budi kuhakikisha katika mazingira yoyote yale, haki za mtoto za kuishi na maendeleo, faragha, ulinzi, uhuru wa kufikiri na kujieleza yanapewa umuhimu wa juu.

Suala la kuzingatia ni kutambua kwamba watoto wanawategemea watu wazima kwa chakula, makazi, uangalizi, ulinzi na ustawi wao kwa ujumla.

Wanahabari hawana budi kufuatilia, kuchunguza na kuchapisha/kutangaza habari za watoto kutoka pande zote kwa kuzingatia misingi ya habari hizo kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

### Watoto waishio katika taasisi:

Hawa ni watoto wanaoishi chini ya uangalizi wa taasisi zilizoidhinishwa zikiwamo shule, hospitali, vituo vya yatima, mahabusu za watoto na hata chini ya ulinzi wa polisi.

- Ni watoto wangapi wako kwenye vituo vya yatima au mahabusu? Wameandikishwa rasmi? Wanaangaliwa na wafanyakazi/wataalamu wenye stadi? Kuna utaratibu wowote wa kufuatilia au kuchunguza na kutoa taarifa za udhalilishaji? Kuna rasilimali za kutosha? Kutoka Serikalini au Asasi za Kiraia? Nini kinatokea watoto hao wanapokua na kufikisha miaka 18 au zaidi?

### Watoto wasio na makazi:

Hawa ni watoto wasio na makazi ya kudumu kutokana na migogoro ama ukatili ndani ya familia, majanga ya asili,

mazingira ya kuishi yasiyo salama, vita n.k.

- ❖ Habari yako inawaelezeaje watoto hawa? Unazingatia mawazo/maoni yao katika kuandika habari zao? Unaelezea vipi usalama na maslahi yao? Nini mchango/wajibu wa wazazi/walezi? Taasisi za Serikali? Mtazamo wajamii?

## Watoto katika uhalifu:

Hawa ni watoto waliovunja sheria.

- ❖ Katika kuandika habari, unawaonyeshaje au unajenga taswira gani ya watoto wahalifu? Unawatambulishaje? Mfumo wa sheria nchini ukoje? Jamii inawachukuliaje? Wasimamizi wa sheria je? Kuna mipango yoyote ya kuwarekebisha?

## Utumikishaji wa watoto:

Hawa ni watoto wanaoajiriwa/kulazimika kutumikishwa kazi ngumu ili kukidhi mahitaji yao au kusaidia wadogo zao au familia zao. Wanaajiriwa katika ajira mbaya ikiwamo ya kufanyakazi za ndani, watoto wanaotumikishwa kingono, omba omba mitaani, n.k.

- ❖ Chunguza kwa makini aina mbaya za utumikishaji wa watoto; kama kuosha magari, kuuza bidhaa mitaani na wale wanaofanyishwa kazi migodini na mashambani. Vyombo vya dola/familia vinashughulikia vipi suala hili? Je, jamii inaelewa matokeo na athari ya kazi ngumu kwa mtoto?

## Watoto wenye ulemavu:

Kundi hili ni lile la watoto wenye mtindio wa ubongo au ulemavu wa viungo wanaohitaji ulinzi maalum ili kuhakikisha utu wao, ukuaji wa kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika shughuli za jamii inayowazunguka.

- Hawa ni watoto ambao wako katika hatari ya kukumbana na aina zote za udhalilishaji. Je, jamii inawachukuliaje? Serikali je? Wanapataje huduma za jamii? afya, elimu, usafiri na huduma nyingine za jamii? Je, sauti yao inasikika? Wanapewa misaada ya kifedha?

## Watoto waliotelekezwa:

Hawa ni watoto ambao wameachwa pweke bila ulinzi, makazi, usimamizi, uangalizi, upendo na hata chakula. Watoto hawa wanaweza kutoka katika familia maskini au tajiri; yatima au watoto wa ndugu.

- Mara nyingi wazazi wa familia maskini, hulazimika kufanya kazi mbali na nyumbani, hivyo huwaacha watoto peke yao nyumbani, wakati baadhi ya wazazi wenye uwezo huachia jukumu la uangalizi wa watoto kwa vitu kama luninga na michezo ya mitandaoni.
- Watoto yatima na wanaolelewa na ndugu, mara nyingi wananyanyaswa kwa kutopewa uangalizi na usalama wa kutosha.
- Je, umewahi kuzungumzia masuala hayo kwenye chombo chako cha habari? Kwa nini hiyo inatokea? Sheria ya familia inafanyaje kazi? Mnawasaidiaje watoto waliotelekezwa na wale wanaozaliwa nje ya ndoa?

## Watoto wasio na makazi

Hawa ni watoto ambao familia zao zimewaacha nyuma kwa sababu mbali mbali ikiwamo kukimbia machafuko, njaa, majanga ya asili, n.k.

- Je, Serikali inawachukuliaje? Jamii je? Kuna mifumo na sera mahususi za kuwalinda na kuwahudumia mahitaji yao ya msingi?

## Watoto Wahamiaji

Hawa ni waloe wanaoishi kwenye makambi na wazazi

wahamiaji ambao hawakuzaliwa kwenye nchi ya makazi hayo ya wakimbizi.

- ❖ Nchi husika inafanya nini kuwalinda watoto hawa? Wana fursa ya kwenda shule? Kupata huduma za afya, chakula, nguo na malazi? Wanalindwa dhidi ya aina zote za udhalilishaji?

## Watoto waishio katika sehemu zenye migogoro/vita

Hawa ni watoto wenye umri chini ya miaka 18 wanaoshiriki katika vita au waliolazimishwa kujiunga na jeshi kama askari.

- ❖ Je, wanalindwa dhidi ya athari za vita? Kabla, wakati na baada ya vita? Unalinda vipi utambulisho wa watoto walioshuhudia ukatili? Unawapa hadhi ya utu au unawajengea taswira ya waathirika wa kimya kimya? Je kuna mipango yoyote ya kuwaondoa kwenye mazingira waliyopo au kuwajenga ili wawe raia bora?

## Watoto wanaoishi na Virusi vya Ukimwi

Hawa ni watoto ambao wanaishi na maambukizi ya VVU au wanaougua UKIMWI.

- ❖ Je, wanalindwa vipi dhidi ya aina zote za ubaguzi? Wanatendewa vipi na taasisi, shule, hospitali? Jamii? Baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwaficha ukweli watoto wanaozaliwa na VVU. Je, watoto hujisikiaje mara wanapotambua kuwa wanaishi na VVU? Sera ya Taifa ya Ukimwi/Sheria inasemaje?

# SEHEMU YA 4: HAKI NA WAJIBU WA MTOTO

## A. HAKI ZA MTOTO

(i) Haki ya Kuishi. Hii inahusu kulinda na kuendeleza uhai wa mtoto ikiwamo:

- Kuzuia magonjwa na kupata huduma za matibabu, chanjo na kufuatilia ukuaji
- Lishe bora
- Mavazi yanayositiri
- Makazi salama
- Maji safi na salama
- Usafi wa aina zote

(ii) Haki ya Kuendelezwa. Maendeleo ya mtoto kiakili yanajumuisha;

- Elimu (rasmi na isiyo rasmi)
- Tamaduni, mila na desturi sahihi za jamii yake
- Kujengwa kiroho na kukuza vipaji

(iii) Haki ya kulindwa; Kuhakikisha mtoto analindwa dhidi ya;

- Unyanyasaji na ubaguzi
- Ukatili (kimwili, kingono na kihisia)
- Unyonywaji ikiwa ni pamoja na ajira za utotoni
- Ukeketaji, ndoa za utotoni na ukatili wa kijinsia
- Mazingira hatarishi
- Kutelekezwa au kuachwa bila mlezi

(iv) Haki ya kushiriki: Kundi hili linahakikisha kwamba;

- Watoto wanapatiwa nafasi ya kutoa mawazo yao
- Maoni yao yanazingatiwa hasa katika uamuzi unao athiri maisha yao
- Mtoto anapaswa kushirikishwa ngazi zote kuanzia

kwenye familia, jamii na Taifa.

## B. WAJIBU WA JUMLA WA MTOTO

Mtoto ana haki, lakini pia ana wajibu. Je, wajibu wa mtoto ni upi? Pamoja na haki za kulinda ustawi wa mtoto, mtoto atakuwa na wajibu na jukumu la;

(a) Kufanya kazi kwa ajili ya mshikamano wa familia.
(b) Kuwaheshimu wazazi, walezi, wakubwa wake na watu wazima muda wote na atawasaidia pale inapohitajika.
(c) Kuhudumia jamii yake na Taifa lake kwa uwezo wake wote kimwili na kiakili kadiri ya umri na uwezo wake.
(d) Kutunza na kuimarisha mshikamano wa jamii na Taifa.
(e) Kutunza na kuimarisha mambo mema katika utamaduni wa jamii na Taifa kwa ujumla katika uhusiano wake na wanajamii.

# SEHEMU YA 5: MIONGOZO YA MAADILI NA KANUNI

Miongozo ifuatayo ni kwa ajili ya kuwasaidia wanahabari kuinua viwango vya weledi ili kuhudumia maslahi ya umma bila upendeleo, kwa usahihi na umakini zaidi bila kuathiri maslahi na ustawi wa mtoto.

## 1.0 Ukweli

1.1 Zingatia ukweli; Upotoshaji wa ukweli kwa namna yoyote ile ili kufanya habari ivutie na hivyo kuuzika zaidi, haukubaliki.

1.2 Acha maigizo. Usiwahadae watoto kusudi wakupatie taarifa au kufanya jambo ambalo si sehemu ya habari yao wenyewe.

## 2.0 Usahihi

2.1 Hakiki mwenyewe habari inayotolewa na watoto na uchukue tahadhari kubwa kuhakikisha uhakiki wako unafanyika bila kuwaweka katika hatari wale wanaokupatia habari za watoto.

2.2 Andika habari kwa usahihi zaidi kadiri inavyowezekana kulingana na muda uliowekwa wa maandalizi ya habari hiyo na nafasi iliyopo na tafuta vyanzo vinavyoaminika.

2.3 Kusanya taarifa kwa uaminifu, tafsiri na andika habari za masuala ya watoto kwa kuzingatia kanuni na kuheshimu haki za mtoto kama zinavyoelezwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto(1999), Sheria ya Ulemavu ya Tanzania ya Mwaka 2010, Sheria ya Ndoa ya Kimila 1971/2019 na sheria/nyaraka nyingine za kikanda na kimataifa kuhusu haki za binadamu.

2.4 Hakiki usahihi wa kile ambacho mtoto amesema mwenyewe, kwa kutumia watoto wengine au mtu mzima. Ingefaa zaidi uhakiki huo ufanyike na pande zote mbili.

## 3.0 Haki

3.1 Tumia njia za haki, uwazi, ukweli za moja kwa moja na kiurafiki kupata habari, picha nzuri na nyaraka na upate vyote hivyo kwa maarifa na ridhaa ya watoto wenyewe au mtu mzima anayehusika, mlezi au mwangalizi.

3.2 Wapatie wazazi/walezi wa mtoto husika haki ya kuuliza maswali, kutoa ufafanuzi wowote au kurekebisha kasoro zilizojitokeza kabla ya kuandika habari; wape fursa ya kujibu lawama zilizoelekezwa kwa mtoto.

3.3 Epuka kuandika habari zitakazoathiri maisha ya mtoto.

3.4 Sahihisha mara moja makosa, upotoshaji au kubadili ukweli wa taarifa.

3.5 Wape watoto sauti, haki na fursa ya kueleza maoni yao kupitia vyombo vya habari bila ushawishi wa aina yoyote ile.

## 4.0 Kutopendelea

4.1 Himiza ubunifu wa mawazo baina ya watoto. Wawezeshe watoto kuelezea kwa ufasaha maoni yao juu ya masuala yanayohusu maisha yao.

4.2 Uliza maswali rahisi na ya moja kwa moja ili mtoto aelewe

4.3 Habari kuhusu madhila ya watoto zisitiwe chumvi au kutolewa maelezo ya kupitiliza. Epuka propaganda, maneno yasiyoeleweka au lugha chafu.

4.4 Habari za watoto zisaidie Kukuza maadili, tunu, mila na tabia njema inayokubalika katika jamii.

## 5.0 Faragha na usiri

5.1 Pata ruhusa kutoka kwa mtoto/mzazi/mwangalizi au mlezi kufanya mahojiano yoyote na watoto na unapotaka kuwapiga picha za kawaida au za video, kuchukua sauti zao kutoka kwenye mikanda, filamu au video nyingine. Na kila inapowezekana, ruhusa hiyo iwe kwa maandishi.

5.2 Hakikisha kwamba mtoto na mlezi hawashawishiwi kwa njia yoyote ile na kwamba kwa hiyari yao, wanaelewa na kukubali kuwa sehemu ya habari hiyo ambayo huenda ikasambazwa kwa

kuchapishwa au kutangazwa.

5.3 Kwa uelewa mzuri zaidi, tumia lugha rafiki kwa mtoto.

5.4 Toleo lolote litakalochapishwa kuhusu maisha ya faragha ya mtoto bila ridhaa yake haliwezi kuhalalishwa kwa sababu tu ya sifa mbaya ya mtoto husika, rekodi ya uhalifu au nafasi ya wazazi wake.

5.5 Tayarisha mazingira ya utulivu na urafiki kabla ya mahojiano. Jadiliana na umhakikishie mtoto kwamba hutatoa utambulisho wake katika kuandika habari hiyo.

6.0 Uwajibikaji

6.1 Dumisha utamaduni wa uwazi na uwajibikaji hasa pale unapopokea, kusimamia na kusambaza habari zinazohusu watoto;

6.2 Ushawishi wa ziada usitumike kupata mahojiano na mtoto/mzazi au mlezi.

6.3 Wezesha utayarishaji bora wa vipindi rafiki vya mtoto na makala rafiki za mtoto.

6.4 Himiza, kuza na kuunga mkono watoto wenyewe kuandika/kutayarisha/kuandaa/kusambaza vipindi na makala zinazowahusu.

6.5 Shawishi wamiliki wa vyombo vya habari kutenga nyenzo, nafasi/muda kwa ajili ya vipindi na makala rafiki za watoto.

6.6 Himiza uanzishwaji wa kamati za kusimamia haki na ustawi wa mtoto katika jamii.

## 7.0 Mahojiano

7.1 Fanya tathmini ya viashiria vya hatari kabla ya mahojiano. Zingatia manufaa au maslahi ya mtoto unapochagua mazingira na mahali yatakapofanyika mahojiano hayo na jinsi yatakavyoendeshwa.

7.2 Kwa kuanzia, kutana na mtoto ukiwa huna kamera au daftari ili mfahamiane na kumjengea mazingira ya utulivu.

7.3 Eleza madhumuni ya mahojiano hayo na matumizi yake. Mpatie mtoto heshima ambayo ungempa mtu mzima;

7.4 Kabla ya mahojiano, jadiliana na umhakikishie mtoto/mzazi/mlezi kuhusu usalama wakati wa mahojiano.

7.5 Unapokuwa na mashaka juu ya usalama wa mtoto wakati wa mahojiano yenu, andika kuwa habari hiyo inajumuisha watoto wote na siyo mtoto mmoja.

7.6 Epuka kutangaza/kuchapisha picha zinazomuonyesha mtoto kama mtu mwenye hatia, au habari inayomvunjia heshima.

7.7 Himiza matumizi ya Mwongozo wa Mzazi (Parental Guidance) kwenye program nyeti za luninga, zikiwamo katuni na vikaragosi vinavyoonyesha ukatili na kutumia lugha chafu.

7.8 Kuwa makini: si habari zote zina maslahi au zinastahili kwa mtoto.

7.9 Epuka kumhoji au kumpiga picha mtoto mwenye umri chini ya miaka 18 bila ridhaa ya mzazi au mtu mzima mwingine mwenye dhamana na mtoto huyo.

7.10 Kwa shuleni, usimhoji wala kumpiga picha mtoto mwenye umri chini ya miaka 18 bila uwepo wa wakuu wa shule au bila ridhaa yao.

8.0 Ubaguzi

8.1 Usiwabague watoto kwa misingi ya jinsia yao, mbari, umri, dini, lugha; hadhi ya kijamii, kiutamaduni na uchumi au uwezo wa kielimu na kimwili;

8.2 Katika kuandika habari zingatia mitazamo mbalimbali kadri uwezavyo, inayohusu hali za watoto kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

8.3 Epuka ubaguzi dhidi ya watoto wenye ulemavu wa akili na viungo. Chukua hatua za ziada kukuza na kulinda heshima na utu wao, na kuwahimiza kujitegemea na kushiriki katika shughuli za maendeleo ya jamii.

## 9.0 Mawazo mgando

Epuka matumizi ya lugha ya mazoea, kama kuwapa watoto majina ya ujumla kutokana na historia zao. Piga vita mitizamo hasi iliyojengwa kwa misingi ya utamaduni, rangi, kabila, na jinsia. Toa haki sawa kwa watoto wa kike na wakiume katika habari unazoandika.

## 10.0 Unyanyapaa/Mshituko

10.1 Zingatia madhara yanayoweza kusababishwa na chapisho au habari inayohusu watoto na epuka unyanyapaa.

10.2

Ficha jina au utambulisho mwingine wa mtoto ambaye ni mhanga wa ukatili au shambulio la kingono, utumikishaji, aliyeshitakiwa au kuhukumiwa kwa uhalifu.

10.3 Epuka kuuliza maswali, kuonyesha mwenendo, kutoa maoni au kauli zinazohukumu, zisizojali miiko ya kitamaduni, zinazoweza kumfedhehesha mtoto au kufufua machungu na huzuni kutokana na matukio au madhila yaliyopita.

## 11.0 Utambulisho

11.1 Ficha utambulisho wa mtoto; epuka kutoa maelezo yasiyo ya lazima yanayomhusu mtoto pale anapotenda au kutendewa uhalifu.

11.2 Jitambulishe mara moja kwa mtoto, wazazi/walezi au wakuu wa serikali katika eneo ulipo na kuomba msaada wao;

11.3 Toa utambulisho wa mtoto iwapo tu ni kwa manufaa ya mtoto husika. Zingatia kuwa mtoto lazima alindwe dhidi ya madhara na kusaidiwa dhidi ya unyanyapaa au visasi.

11.4 Hakikisha kuwa mtoto hatokuwa katika hatari wala kuathiriwa kwa kutangaza kwako makazi yao, jumuiya au mahali walipo;

11.5 Hakiki vitambulisho vya shirika lolote linalodai kuzungumza kwa niaba au kwa kuwakilisha maslahi ya watoto;

11.6 Linda utambulisho wa mtoto au wazazi/walezi isipokuwa pale tu itakapoonekana ni kwa ajili ya manufaa ya mtoto;

11.7 Usichapishe habari au picha yoyote ambayo inaweza kumuweka katika hatari mtoto, wadogo zake au wanarika wenzake hata kama utambulisho wao ulibadilishwa, kufichwa au haukutumika;

11.8 Usieneze habari za watoto wanaoishi katika mazingira magumu bila ridhaa/ruhusa yao;

11.9 Katika mahojiano ya filamu, video na radio, zingatia namna uchaguzi wa matumizi ya vielelezo, iwe picha au sauti

unavyoweza kuathiri maisha ya mtoto.

## 12.0 Punguza Madhara

12.1 Katika tukio ambapo mtoto anasimulia hadithi ya huzuni, usioneshe wazi kumhurumia kwani hiyo inaweza kufufua hisia za machungu yaliyopita;

12.2 Kabla ya kuchapisha au kutangaza habari, hakikisha inakidhi viwango vya juu vya uandishi wa habari kwa kuzingatia uwiano, usawa na usahihi kiasi kwamba hakuna mtoto au mzazi/mlezi atakayejutia kuchangia utengenezaji wa habari hiyo.

## 13.0 Teknolojia Mpya

Katika miaka ya hivi karibuni, aina mpya za mawasiliano kwa mitandao ya kijamii kama Internet, Twitter, Blogs, Skype, TikTok, Snapchat, Instagram, WhatsApp na Facebook yameleta hali ya wasi wasi kote duniani. Wanaodhalilisha watoto kingono wamekuwa wakitumia mitandao hiyo kunyemelea watoto na kusambaza picha za utupu za watoto.

13.1 Linda watoto kwa kukagua taarifa za mitandao ya kijamii kuhakikisha hazina udhalilishaji wa watoto.

13.2 Tetea matumizi ya namba ya simu ya dharura ya kutoa taarifa za udhalilishaji wa mtoto.

13.3 Piga vita matangazo/udhamini wa vipindi vya watoto unaofanywa na makampuni ya sigara na pombe.

13.4 Pinga matangazo nyeti ya video na filamu yanayotumia watoto.

14.0 Faida Binafsi

14.1 Epuka kufanya malipo yoyote kwa ajili ya vifaa vya watoto au vitu vinavyohusu ustawi wao kupitia kwa wazazi/walezi isipokuwa tu kama itaonekana ni kwa manufaa ya mtoto.

## Rejea


1. Sheria ya Mtoto (2009)-Tanzania
2. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto, (1999).
3. Ulinzi wa Mtoto na Vyombo vya Habari – Save the Children Tanzania (2010)
4. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (CRC)-1989
5. Katiba ya Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania (1977).
6. Maadili ya Vyombo vya Habari naMwongozo wa Kuandika Habari dhidi ya Udhalilishaji wa Mtoto (MWAs 2008).
7. Taasisi ya Vyombo vya Habari Philippines-UNICEF (2011)
8. Vyombo vya Habari na Haki za Watoto - UNICEF (2005)
9. Watoto katika Haki – Miongozo ya Waandishi wa Habari-Shirikisho la Kimataifa la Waandishi wa Habari-IFJ(2002)
10. Habari za Watoto: Miongozo- Malaysia (2007)
11. Ulinzi na Usalama wa Mtoto ni Jukumu Letu Sote – World Vision – Tanzania & Christian Council of Tanzania (CCT) – 2018
12. Ulinzi na ustawi wa mtoto, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 - World Vision Tanzania (December 2014)

Media Council of Tanzania (MCT)
House No. KUN/MTN/532, Bagamoyo Road, Tegeta Skanska Area,
P. O. Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania. | Mob: +255 719 494 640/+255 767 494 826
Website: https://www.mct.or.tz

ISBN: 978-9976-588-01-9

mediacounciltanzania mediacounciloftanzania mctanzania mediacounciloftanzaniamct